UHURU UK 18.

# Mradi machinjio mapya ya Vingunguti waiva

**Na CHRISTOPHER LISSA**

BARAZA la Wazee la Mkoa wa Dar es Salaam limeeleza kuridhishwa na ujenzi wa machinjio ya mapya ya Vingunguti huku vifaa vya kisasa vikitarajiwa kuwasili nchini Julai 15, mwaka huu.

Hayo yalijiri wakati ziara ya viongozi na wajumbe wa baraza hilo ya kukagua maendeleo ya ujenzi wa machinjio hiyo, ambapo walimpongeza Rais Dk. John Magufuli kwa utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi Chama Cha Mapinduzi (CCM).

Katibu wa Baraza hilo, Mohammed Mtulia, alisema dhamira ya ziara yao ilikuwa ni kujionea utekelezaji wa Ilani katika mradi huo wa kimkakati ambao utakuwa chachu kubwa katika kuinua uchumi na kuongeza ajira.

"Tumeridhishwa na ujenzi huu na baraza linapongeza kazi kubwa iliyofanywa na serikali ya awamu ya tano chini ya Rais Dk. Magufuli katika kuhakikisha mradi huu unakamilika," alisema Mtulia.

Mjumbe wa Baraza hilo na Mwenyekiti wa Baraza la Wazee Wilaya ya Temeke, Mohammed Bonde, alisema kukamilika kwa machinjio hayo ni utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya CCM.

> **Tumeridhishwa na ujenzi huu na baraza linapongeza kazi kubwa iliyofanywa na serikali ya awamu ya tano chini ya Rais Dk. Magufuli katika kuhakikisha mradi huu unakamilika.**
>
> Mohammed Mtulia, Katibu wa Baraza la Wazee Dar es Salaam

Diwani mstaafu wa Kata ya Vingunguti, Omari Kumbilamoto, alisema mradi uko katika hatua za mwisho kukamilika na utaleta ajira nyingi hususan watu zaidi ya 300.

"Ni mradi wenye tija kubwa kwa Taifa lakini zaidi kwa wananchi wa Kata ya Vingunguti ambao mpaka sasa wamenufaika na ajira za ujenzi. Pia kuna fursa kubwa ya ajira rasmi zaidi ya 300 mradi utakapoanza kufanya kazi,"alisema Kumbilamoto.

Alisema mbali na ajira hizo, mradi huo wa machinjio utatoa fursa ya ajira kwa vijana ambao walikuwa wakifanya kazi katika machinjio ya awali ambao wataandaliwa eneo maalumu la kuuza nyama rejareja huku mama lishe nao wakiboreshewa maeneo yao .

Awali, Mhandisi wa Shirika la Nyumba la Taifa (NHC), Mburuga Matamwe, aliwaambia wajumbe wa baraza hilo kuwa vifaa vya kuchinjia ng'ombe na mbuzi vitawasili nchini Julai 15, mwaka huu.

"Vimechelewa kidogo kwa siku 40 kwa sababu ya mlipuko wa virusi vya corona vinavyosababisha homa kali ya Covid-19. Tutafunga mashine hizo kwa siku 30 na tutazijaribu kwa siku 15. Baada ya hapo kazi ya uchinjaji rasmi itaanza," alisema.

Mradi huo unagharimu zaidi ya sh.bilioni 12 zilizotolewa na serikali na Halmshauri ya Manispaa ya Ilala.

Idadi>>Mra

Na MWANDISHI W

NAIBU Katibu M
ya Nishati, M
Masanja, ame
kusambaza umeme
Kampuni ya TEXPOL k
300 za vijiji sita vilivyo
Ilungu, Wilaya ya Uyo
hairidhishi.
Hayo aliyasema b
ziara ya kukagua ka
umeme iliyofanywa
hiyo kwa lengo la k
na kutathmini ubo
miundombinu iliy
kutekeleza kazi ya u
katika eneo husika.
Awali, Kampun
kujenga kituo kidogo
kwa kutumia mapo
katika wilaya hiyo na
wananchi umeme hu
ya serikali, jambo a
kutekelezwa hadi sas
Badala yake kam
kazi ya kusambaz
zinavyofanya kampu
mradi wa usambaz
katika maeneo mbali
Katika ziara hiyo,
huyo aliambatana na
wa Umeme kutoka
Viongozi wengine k

UZINDUZI



WAZIRI wa Ardhi,
Mji, Mhandisi Mo

## DC aha

Na ALLAN KITW

MKUU wa Wilaya ya
Peres Magiri, amew
wa maendeleo n
kujitokeza kuchan
katika vijiji 40 ambav
kuunga mkono juhu
huduma za afya kw
Magiri alibainish
na gazeti hili wilayan
kipaumbele chake
Mkuu wa wilaya hiy
71 vya wilaya hiyo v
Alisema hadi s
zahanati katika vi
dhamira yake ni kuh
vinapata zahanati il
karibu zaidi na wan
Magiri aliagiza
ambavyo havina
mchakato wa uje
maeneo yao kwa

Scanned with CamScanner

Kiuyu Kigongoni Wilaya ya Wete Mkoa wa Kaskazini Pemba.

Ilidaiwa bila ya halali alimbaka msichana mwenye umri wa miaka 17.

NIPASHE UK 9.

# Utotoleshaji vifaranga samaki kuanza

**Mary Mshami na Magdalena Haule**

SERIKALI imesema mradi wa kutotolesha vifaranga vya samaki kwa ajili ya kukidhi soko nchini utaanza hivi karibuni ili kuchochea uchumi wa viwanda.

Mradi huo ni wa usimamizi wa uvuvi wa Kanda ya Kusini Magharibi mwa Bahari ya Hindi (SwioFish), utakaotekelezwa Oktoba, mwaka huu.

Hayo yalisemwa na Katibu Mkuu wa Mifugo na Uvuvi, Rashid Tamatamah, alipotembelea maonyesho ya Sabasaba.

"Mradi kama huu utasaidia kukuza sekta ya viwanda na uvuvi na kutoa elimu kwa wanafunzi ambao watapata fursa ya kujifunza kwa vitendo," alisema Tamatamah.

Alisema mchakato wa ujenzi wa mradi wa maabara ya vifaranga vya samaki Kunduchi umeanza na watashirikiana na Chuo Kikuu cha Dar es Salaam na baada ya miezi mitatu ujenzi utaanza kwa kutumia teknolojia ya kisasa.

Kadhalika, alisema katika maonyesho ya Sabasaba ya mwaka huu, watatoa elimu kwa wavuvi ya kuvua samaki wa kuliwa.

Scanned with CamScanner



# Waziri aagiza kukamatwa madaktari vishoka wa mifugo

**Na Ibrahim Joseph, DODOMA**

WAZIRI wa Mifugo na Uvuvi, Luhaga Mpina, ameagiza kukamatwa kwa madaktari wa mifugo vishoka ambao hawana ujuzi wa kutoa huduma za afya ya mifugo.

Aidha, ametoa maagizo 25 kwa bodi tatu zinazohusika mifugo na uvuvi huku akisema wataoshindwa kutekeleza uteuzi wao utatenguliwa wakati wowote.

Mpina alitoa agizo hilo alipokuwa akizungumza na wajumbe wa kuzindua bodi ya Wakala wa Vyuo vya Mafunzo ya Mifugo (LITA), Baraza la Vetenari Tanzania (VCT) na Bodi ya Hifadhi za Bahari na Maeneo Tengefu (MPRU).

Aliagiza bodi hizo kuhakikisha zinasimamia vizuri maadili ya madaktari kwa kuwakamata vishoka wote ambao wanatoa huduma za afya za mifugo nchini huku wakijua kuwa hawana ujuzi huo.

"Kuanzia leo natoa agizo na katazo kwa watu wasio na sifa yaani vishoka ya kutoa huduma za afya ya wanyama ni marufuku kabisa katika nchi yetu, tena tukikutana na mtu anaitwa kishoka nisiendelee kulisikia," alisema.

Alisema katika marekebisho ya sheria ambayo yanafanyika yanatakiwa yaendane na hasara ambayo kishoka anatakiwa kumlipa mfugaji kutokana na hasara aliyoisababisha kwa kutoa dawa au tiba isiyostahili.

"Adhabu ya kulipa faini haitoshi kishoka anatakiwa amlipe fidia mfugaji wetu aliyepata hasara ya mifugo yake kufa kwa sababu amedanganywa na kishoka huyo," alisema.

Alibainisha kuwa mtu ambaye hajasomea fani husika ataweza kutoa dawa kwa kuzidisha dozi au na kusababisha vifo vya mifugo.

Alisema mabaraza hayo yahakikishe yanaboresha huduma za afya za wanyama kwa kushirikiana na sekta binafsi wahakikishe wafugaji wanapata huduma sahihi.

Pia, aliyaagiza mabaraza hayo yote kuhakikisha wanasimamia ukusanyaji wa mapato na maduhuli yote ya serikali angalu kufikia makusanyo ya Sh. bilioni moja kwa mwaka tofauti na yaliyokuwapo ya Sh. milioni 251 kwa sasa.

Aidha, aliagiza mabaraza la vetenari kuwafuta kwenye orodha za madaktari, madaktari wote ambao hawajalipa ada zao kulingana na sheria walizojiwekea.

Alisema kama daktari hataki kulipa ada maana yake anajitoa kwenye orodha ya wataalamu hao kwa mujibu wa masharti waliojiwekea, na ndio maana anasababisha uwepo wa vishoka.

Naye Katibu Mkuu wa Wizara hiyo (Mifugo), Prof. Elisante Ole Gabriel, aliwataja viongozi wa bodi hizo kuwa ni Prof. Mkongo Mlozi wa LITA, Dk. Bonaventura Baya wa MPRU na Prof. Kazwala Rudovick Baraza la Vetenari anaendelea.

Kwa upande wake, Prof. Mlozi alimshukuru waziri kwa uteuzi wao na kuahidi kuyafanyia kazi maagizo aliyotoa kwao.

Alisema timu hiyo iliyoteuliwa itaanza vikao vyake haraka ili kufanya utekelezaji wa maagizo hayo ambayo ndiyo dira ya kazi.



Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Luhaga Mpina, akizungumza wakati akizindua bodi tatu za wizara hiyo jijini Dodoma juzi. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

Scanned with CamScanner

# PICHA YA SIKU: MAMBO YA MNADANI

Mchuuzi akiandaa nyama kabla ya kuiuza kwa wateja katika eneo la mnada wa Kibirashi uliopo Wilaya ya Kilindi mkoani Tanga jana. Mtanda huo hufanyika kila Jumanne. **Picha na Rajabu Athumani**



Scanned with CamScanner

customers' products and services. policies. This is a complete promote greater regulatory compatibility with US rules and prices or supplies," the CSOs maintained.

ıre
se

sub-
next
ging
AIDS
per
e an

HIV
cess
nnot
took
ome
we
ces,
and
d to
said
ient
of
ome
ces
uch
ion
ing
HIV

ing
-19,
are
a
19,
by
ers
all



Livestock and Fisheries minister Luhaga Mpina speaks at Monday's launch in Dodoma city of boards of directors of three agencies under the ministry: Livestock Training Agency, Veterinary Council of Tanzania, and Marine Park and Reserves Unit. Photo: Correspondent Ibrahim Joseph

maize which have been given to the ward councillor," he stated.

He said the maize will be given to Loltepes primary school in Kiteto

**given to the ward councillor**



People visiting the DITF use automated teller machine services at the NMB Bank Plc pavilion, as found yesterday. Photo: Guardian Correspondent

THE GUARDIAN.

# Mpina orders arrest of fake veterinary officers

**By Guardian Correspondent, Dodoma**

LIVESTOCK and Fisheries minister Luhaga Mpina has ordered the arrest of veterinary officers who lack required skills.

He also gave 25 directives to three livestock and fisheries boards saying those who will fail to implement the directives, their appointments will be revoked any time.

Mpina issued the directives here yesterday when speaking to newly appointed board members in Livestock Training Agency (LITA), Veterinary Council of Tanzania (VCT) and Marine Parks and Reserves Unit (MPRU).

He instructed all these boards to ensure they supervise veterinary officers' ethics by arresting fake veterinary officers who provide veterinary services to the livestock in the country while knowing they are not qualified to do so.

He said the ongoing amendment of the laws must go in tandem with the loss which a fake veterinary officer has caused to the livestock owner by prescribing wrong drugs, adding that fining them was not adequate, the fake veterinary officer must pay the livestock owner the loss of his animals.

He also directed the boards to increase government revenues that has to at least reach 1bn/- per year from the current 250m/-.

Mpina also instructed the deregistration of all veterinary officers who have not paid their fees in accordance with the law.

The ministry's Permanent Secretary Prof Elisante Ole Gabriel mentioned the Board Members including Prof Mkongo Mlozi (LITA) Dr Bonaventura Baya (MPRU) and Prof Kazwala Rudovick (VCT).

Prof Mlozi thanked the minister for their appointment and pledged to work on the directives issued.


**KILIMANJARO NATIVE CO-OPERATIVE UNION (1984) LIMITED**
**(KNCU (1984) LTD)**
**REG.NA.4054**

WASHINGTON STATE UNIVERSITY
The Paul G. Allen School for Global Animal Health